# VIJANA Magazine

Toleo la Machi, 2026




UMOJA WA VIJANA WA CCM

www.uvccmtz.or.tz

@uvccm_tz// UVCCM TV

**HALIUZWI**

# Yaliyomo

Kwenye Vijana Magazine




**01.** *Rais Samia Amuasili mtoto aliyetelekezwa, atoa wito*

**03.** *Rais Samia Afuturisha Mabalozi, Ikulu DSM*

**04.** *Rais Mwinyi: Futari ya Kitaifa Znz ni historia ya Umoja*

**06.** *Dkt. Migiro ahimiza matumizi ya AI na Ubunifu ndani ya CCM*

**08.** *Kawaida aongoza Dua Maalum kuwaombea Dkt. Samia, Mwinyi*

**10.** *Katibu Mkuu Mwinyi akagua Chuo cha Vijana - Ihemi*

**12.** *Manaibu Katibu Wakuu UVCCM Waiwakilisha Tanzania, Zimbabwe*

**13.** *Waziri Mkuu akagua ukarabati wa Uwanja wa Ndege S'wanga*

**15.** *Uchaguzi wa Senet wafanyika Nchi nzima, Mikoa 30 yahusika*

**17.** *Dkt. Bunungu ang'ara Uchaguzi Mdogo - Peramiho*

**19.** *Siku 100 za Dkt. Samia zimeleta fursa na matumaini kwa Vijana*

**23.** *Dkt. Samia mdau Na. 1 michezo nchini*


Kazi na Utu Tunasonga Mbele

# DIBAJI

## Karibu kwenye VIJANA Magazine: Nguvu ya Kijana, Uhai wa Taifa!

Kwa niaba ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) na vijana wote wa Tanzania, tunayo furaha kubwa kukukaribisha kwenye jarida letu maalum, Vijana Magazine.

Jarida hili siyo tu sehemu ya habari, bali ni jukwaa la matumaini, ari, na maono ya Vijana wenye dhamira ya kuleta mabadiliko chanya katika Taifa letu.

Katika toleo hili, tunajivunia kuangazia hatua kubwa zilizopigwa chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Viongozi hawa wameonesha dhamira ya kweli katika kujenga taifa lenye fursa, mshikamano, na ustawi kwa wote.

Jarida hili linaangazia miradi yenye athari chanya kwa maisha ya vijana na watanzania wote kuanzia elimu na afya hadi nishati na uchumi wa viwanda. Zaidi ya hayo, tunasisitiza nafasi muhimu ya vijana kama nguvu ya taifa, tukichochewa na uzalendo, maadili, na bidii.

Tunatambua na kuthamini juhudi za viongozi wetu, wanachama wa CCM, na vijana wote wanaochangia kujenga Tanzania ya maendeleo na usawa. Ushirikiano wenu ni nguzo kuu ya mafanikio tunayoyashuhudia leo na tunayokusudia kufikia.

Vijana Magazine ni yako, ni yetu, ni sauti ya kizazi cha matumaini.
Hebu tuendelee kuwasha mwanga wa kijani, tukilenga maendeleo endelevu kwa wote.

## KULINDA NA KUJENGA UJAMAA

*Ndugu Mohammed Ali Kawaida (MCC)*
*Mwenyekiti wa Jumuiya ya UVCCM*



# RAIS SAMIA AMUASILI MTOTO MCHANGA ALIYETELEKEZWA, ATOA WITO KWA JAMII

Na Mwandishi wetu,
Dodoma

Katika tukio lililogusa hisia za wengi na kuibua tafakari kuhusu thamani ya maisha ya watoto, Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan amemkaribisha katika familia yake mtoto mchanga wa kike aliyepatikana akiwa ametelekezwa mjini Nzega, akiahidi kumpatia malezi bora, ulinzi na huduma zote muhimu kwa ukuaji wake.

Mtoto huyo, aliyepewa jina la Grace Samia Suluhu Hassan, alikabidhiwa rasmi Tarehe 11 machi 2026 katika makazi ya Ikulu ya Chamwino na Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Naitapwaki Tukai, baada ya kupita katika hatua mbalimbali za uangalizi tangu alipopatikana mapema Januari 17, 2026

Akieleza mazingira ya kupatikana kwa mtoto huyo, Mkuu huyo wa Wilaya alisema aliokotwa Januari 17, 2026 katika eneo lililo karibu na nyumba ya wageni ya Kasulu, Nzega Mjini, akiwa ameachwa bila mlezi.

Alisema mara baada ya taarifa hizo kupokelewa, mamlaka za wilaya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Tanzania zilichukua hatua za haraka za kumpeleka mtoto hospitalini kwa uchunguzi wa afya na huduma za awali, huku juhudi za kumtafuta mzazi wake zikiendelea kwa kipindi chote bila mafanikio.

"Lengo letu lilikuwa kwanza kuhakikisha usalama wake na afya yake vinapewa kipaumbele, sambamba na kufuata taratibu zote zinazohitajika kisheria," alisema Tukai wakati wa makabidhiano hayo.

Baada ya kumpokea mtoto huyo, Rais Samia alisisitiza kuwa jamii ina wajibu wa kutunza uhai wa watoto na kuhakikisha changamoto zinazowakabili wazazi hazigeuki sababu ya kuhatarisha maisha ya watoto wachanga.



> Wanaotupa watoto hawajui wanalolifanya. Kuliko kumtupa mtoto ni afadhali ukamkabidhi katika mamlaka za kisheria au kituo cha kulelea watoto. Kila mtoto aliyezaliwa ni hazina, na hatuijui kesho yake.

***Dkt. Samia Suluhu Hassan***
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Kauli hiyo ilibeba ujumbe mzito kwa kijamii, ikikumbusha kwamba kila mtoto ana haki ya kuishi, kulindwa na kupewa nafasi ya kukua katika mazingira salama yenye upendo.
Hatua ya Rais Samia imeendelea kutafsiriwa na wengi kama mwendelezo wa uongozi unaojali ustawi wa watu katika nyanja mbalimbali, hususani pale jamii inapokutana na mazingira yanayohitaji mkono wa huruma na maamuzi yenye kugusa maisha ya moja kwa moja.



## *Maoni ya Mwandishi*

Kwa ujumla, tukio hili linaacha funzo pana kwa jamii kwamba thamani ya uongozi haipimwi kwa maamuzi makubwa pekee, bali pia kwa uwezo wa kugusa maisha ya watu katika nyakati nyeti zinazohitaji huruma na uwajibikaji. Kwa sisi vijana, hatua ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inapaswa kutafsiriwa kama wito wa kujenga kizazi kinachothamini utu na kinachotambua kuwa kila mtoto ni tumaini la taifa la kesho. Katika mazingira ya dunia inayobadilika kwa kasi, bado upendo, malezi na mshikamano wa kijamii vinaendelea kuwa msingi muhimu wa taifa lenye maadili, utu na matumaini ya kudumu



# RAIS DKT. SAMIA AFUTURISHA MABALOZI IKULU DAR ES SALAAM

Na Mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 03 Machi 2026 aliandaa futari maalumu kwa Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini pamoja na wakuu wa Mashirika ya kimataifa, hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam.
Tukio hilo lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kidiplomasia kitaifa na kimataifa likiimarisha mahusiano ya kimataifa. Futari hiyo iliyoandaliwa na Rais Dkt.Samia imeendelea kudhihirisha dhamira ya Taifa letu la Tanzania katika kujenga ushirikiano wa karibu na jumuiya ya kimataifa katika nyanja za maendeleo, uwekezaji na ustawi wa jamii.

Pia Balozi wa Comoro nchini Tanzania, Mheshimiwa Ahmada El Badaoui Mohamed Fakih, aliwaongoza wageni waliohudhuria katika dua maalum mara baada ya futari, akitoa shukrani kwa Rais Samia kwa ukarimu na uongozi wake unaojali mahusiano ya kimataifa.







# RAIS DKT. MWINYI: FUTARI YA KITAIFA ZANZIBAR NI HISTORIA YA UMOJA NA MSHIKAMANO

Na Mwandishi wetu,
Zanzibar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa Zanzibar imeandika historia ya kipekee kwa kuandaa Tukio Kubwa la Futari ya Kitaifa kwa mara ya kwanza, lililowakusanya maelfu ya Waumini wa Dini ya Kiislamu katika mkusanyiko wa pamoja.

Alhaj Dkt. Mwinyi ameyasema hayo leo tarehe 07 Machi 2026 alipotoa salamu zake kwa maelfu ya Waumini wa Dini ya Kiislamu waliohudhuria Futari hiyo ya Kitaifa iliyofanyika katika Uwanja wa New Amaan Complex, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Amesema tukio hilo ni jambo jema lenye thawabu kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, sambamba na kuwa jukwaa muhimu la kuwaunganisha Waumini wa Dini ya Kiislamu pamoja na wananchi kwa ujumla katika kuimarisha mshikamano, upendo na umoja.

Aidha, Alhaj Dkt. Mwinyi amezishukuru taasisi za Serikali zilizoshirikiana kufanikisha Futari hiyo ya Kitaifa, ambazo ni Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, Kamisheni ya Utalii Zanzibar pamoja na



Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), kwa juhudi zao za kuandaa tukio hilo kubwa lililowakutanisha Waumini wengi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Katika nasaha zake, Rais Dkt. Mwinyi amewataka Waumini kuendelea kuzidisha ibada, dua na matendo mema katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, huku wakiendelea kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuijalia nchi amani, utulivu na mshikamano miongoni mwa wananchi wake.

Kwa upande wake, Naibu Mufti wa Zanzibar, Sheikh Mahmoud Mussa Wadi, amesema Futari hiyo ya Kitaifa ni tukio muhimu linaloongeza mapenzi na upendo miongoni mwa Waumini, huku likichangia kuondoa chuki na kuimarisha mshikamano kati ya makundi mbalimbali ya Waumini wa Dini ya Kiislamu.





# DKT. ASHA- ROSE MIGIRO AHIMIZA MATUMIZI YA AKILI BANDIA (AI) NA UBUNIFU NDANI YA CCM

Na Mwandishi wetu,
Dodoma

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Asha-Rose Migiro, amewataka watendaji na wanachama wa chama hicho kujenga uwezo na uimara katika kusimamia rasilimali na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa hali ya juu.
Dkt. Migiro amesema hayo akifungua rasmi mafunzo maalum ya Uongozi na Utawala Bora kwa viongozi na watendaji waandamizi wa Chama yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mount Royal, Mkoani Iringa tarehe 09 Machi 2026.

Dkt. Migiro amesisitiza umuhimu wa kwenda na wakati kwa kutumia teknolojia mpya zinazochipukia duniani ikiwemo matumizi ya Akili Bandia (Artificial Intelligence) ambapo amebainisha kuwa ni lazima watendaji waelewe na kutumia Artificial Intelligence (AI) ili kuboresha utendaji kazi na ufanisi wa chama katika zama hizi za kidijitali.
Pia alielezea kuhusu Usalama wa Mifumo ya Kidijitali ambapo amehimiza umuhimu wa kuwa na mifumo imara ya kidijitali na kukabiliana na changamoto za uhalifu wa mitandaoni (cybercrime).





Aidha ameelezea kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya maandalizi ya kuandaa mpango mkakati wa miaka mitano ijayo, utakaosaidia taasisi za chama kukua kwa misingi ya maono ya pamoja huku akigusia utekelezaji wa Ilani akisitiza kuwa chama kipo katika kipindi muhimu cha utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2025-2030, lengo likiwa ni kujenga taifa jumuishi lenye ustawi na haki.






"Lazima tujenge uwezo, tujenge uimara wa kusimamia rasilimali na majukumu yetu kwa ufanisi na uwajibikaji... Ni matumaini yangu kuwa mafunzo haya yatatupa fursa ya kuwasilisha maoni yetu kwenye mpango mkakati wa miaka mitano ijayo,"

Dkt. Migiro.





# MWENYEKITI KAWAIDA AONGOZA DUA MAALUM KUWAOMBEA DKT. SAMIA NA DKT. MWINYI

Na Mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Mwenyekiti wa UVCCM Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Ndugu Mohamed Ali Kawaida, tarehe 12 Machi 2025 aliongoza vijana wa Kitanzania katika dua maalum ya kuwaombea viongozi wakuu wa nchi

Dua hiyo ilihusisha kumuombea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ili waendelee kupewa afya njema na hekima katika kuongoza Taifa.

Tukio hilo lilifanyika Tunguu, Zanzibar, likiwakutanisha vijana wa UVCCM pamoja na wananchi.

Katika tukio hilo, ilielezwa umuhimu wa vijana kuendelea kushiriki katika kumuombea kiongozi wa nchi kama sehemu ya kuimarisha mshikamano, amani na utulivu wa Taifa. Pia, vijana walikumbushwa nafasi yao katika kudumisha maadili na kuchangia maendeleo ya nchi.

Baada ya dua hiyo, shughuli iliendelea kwa tukio la futari ya pamoja (iftar) iliyoandaliwa na UVCCM ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha mwezi mtukufu wa Ramadhani na kujenga mahusiano mema katika makundi ya vijana na jamii yote kwa ujumla ikijikita zaidi katika kuimarisha uhusiano miongoni mwa vijana.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Ndugu Mohamed Said Mohamed (Dimwa), ambapo tukio hilo liliambatana na ujumbe wa kuhimiza mshikamano, uzalendo na ushiriki wa vijana katika shughuli za maendeleo.

Tukio hilo ni wazi Linaakisi mwendelezo wa juhudi za UVCCM katika kuunganisha vijana na kuimarisha misingi ya amani na utulivu nchini.





Habari picha - Iftar ya UVCCM katika Chuo cha Tunguu 2026







# KATIBU MKUU UVCCM, MWINYI AKAGUA MAENDELEO CHUO CHA VIJANA IHEMI - IRINGA

Na Mwandishi wetu,
Dodoma

Katibu Mkuu wa UVCCM na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Ndugu Halid Mwinyi ametembelea na kukagua maendeleo ya Chuo cha Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) cha Ihemi kilichopo mkoani Iringa.

Akizungumza wakati wa ukaguzi huo ukiwa na lengo la kutambua fursa mpya akiambatana na Viongozi wa UVCCM mkoa wa Iringa pamoja na Mbunge wa Vijana mkoa huo, Mhe. Jasmine Chesco amewaeleza kuwa ni muhimu Jumuiya iunganishe siasa na miradi ya kiuchumi.

Chuo cha Ihemi chenye ardhi yenye ukubwa wa mita za mraba 1,963 kikiwa na miradi mchanganyiko ikiwemo fremu za biashara 36, kiwanda cha ushonaji, zana za kisasa za kilimo ikiwemo matrekta, kiwanda cha ushonaji na miradi ya kilimo na mifugo.

Ndugu Mwinyi alikagua uwekezaji wa hekari 38 za kilimo cha parachichi, shamba la mahindi lenye hekari 25, mradi wa kuku, nyuki na kitalu nyumba (greenhouse) na josho la mifugo linalohudumia jamii.


Akiendelea na ukaguzi Ndugu Mwinyi alitembelea bweni lililozinduliwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kuagizia viongozi wa UVCCM mkoa huo kulitunza kuwa sehemu ya kumbukumbua na urithi wa Chama.

Aidha ameagiza kugawiwa hekari 10 kila wilaya ya mkoa wa Iringa ili kufanya uzalishaji na kuendeleza eneo hilo.





Katibu Mkuu akikagua maeneo
Chuo cha Ihemi





# MANAIBU KATIBU WAKUU UVCCM WAIWAKILISHA TANZANIA SHEREHE ZA SIKU YA KIJANA ZIMBABWE




Na Mwandishi wetu,
Dodoma

HABARI PICHA: Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Bara, Ndugu Mussa P. Mwakitinya (kushoto), Waziri wa Uwezeshaji na Maendeleo ya Vijana nchini Zimbabwe, Mhe. Tinoda Machakaire (katikati) ambaye pia ni Mbunge na Mwanachama wa ZANU-PF na Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Zanzibar, Ndugu Abdi Mahmoud Abdi (kulia) wakiwa katika picha ya pamoja nchini Zimbabwe. Manaibu hao walikuwa nchini humo wakiiwakilisha Tanzania katika sherehe ya Siku ya Kijana Zimbabwe ambayo ilihudhuriwa pia na Viongozi Vijana wa Vyama vya Siasa rafiki kutoka nchi mbalimbali Afrika.



# WAZIRI MKUU AKAGUA UKARABATI WA UWANJA WA NDEGE WA SUMBAWANGA

Na Mwandishi wetu,
Dodoma

Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba leo Machi 08, 2026 amekagua maendeleo ya ukarabati na uboreshaji wa Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga uliopo mkoani Rukwa.

Mradi huo ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa gharama ya shilingi bilioni 60.1 na hadi sasa umefikia asilimia 96 ya utekelezaji.

Akizungumza wakati wa ukaguzi huo, Dkt. Mwigulu amewapongeza wananchi wa Rukwa kwa kupata uwanja wa ndege wa kisasa kwa kuwa maendeleo hayo yanaonesha mabadiliko makubwa ya mkoa huo.

Amesema kuwa kwasasa Rukwa siyo ile ya zamani bali ni Rukwa ya kisasa na ya viwango, inayokwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya taifa.

Aidha, amesema miradi ya aina hiyo ndiyo mafanikio ambayo Serikali ya Awamu ya Sita inajivunia kwa kuwekeza katika miradi ya maendeleo yenye tija na inayoacha alama kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Ukarabati na upanuzi wa uwanja huo unatarajiwa kuimarisha huduma za usafiri wa anga katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini pamoja na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ameanza ziara ya kikazi katika mkoa wa Rukwa ambapo atakagua miradi ya maendeleo pamoja na kuzungumza na wananchi.






Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga



# UCHAGUZI WA SENETI UVCCM WAFANYIKA NCHI NZIMA, MIKOA 30 YAHUSIKA

Na Mwandishi wetu,
Dodoma

Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) kupitia Idara ya Uhusiano wa Kimataifa kwa Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu, umeratibu na kusimamia kwa mafanikio mchakato wa uchaguzi wa Seneti katika mikoa 30 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, zoezi la uchukuaji wa fomu kwa wagombea lilitangazwa rasmi kati ya Januari 5 hadi 7, 2026, ambapo sifa za wagombea zilielezwa wazi ili kuhakikisha upatikanaji wa viongozi wenye sifa stahiki. Miongoni mwa vigezo vilivyowekwa ni pamoja na mgombea kuwa mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuwa mwanafunzi aliyedahiliwa katika taasisi ya elimu ya juu na kuwa na muda wa kutosha wa masomo uliobaki.

Aidha, wagombea walitakiwa kuwa wazalendo kwa Chama cha Mapinduzi, huku wanafunzi wa ngazi mbalimbali wakiwekewa viwango maalum vya miaka ya masomo ili kuweza kugombea nafasi hizo.
Katika Tanzania Bara, uchaguzi huo ulifanyika katika mikoa ikiwemo Arusha, Dar es Salaam,





Dodoma, Mwanza, Mbeya, Morogoro, Tanga, pamoja na mingineyo, wakati Zanzibar ulifanyika katika mikoa ya Kusini Unguja, Magharibi, Kusini Pemba, Kaskazini Pemba na Mjini.

Hata hivyo, uchaguzi haukufanyika katika baadhi ya maeneo. Mkoa wa Kaskazini Unguja haukushiriki kutokana na kukosekana kwa vyuo vya elimu ya juu, huku Mkoa wa Geita ukikosa uchaguzi huo kwa kuwa ni mkoa mpya ambapo Seneti imeanzishwa mwaka huu. Badala yake, maandalizi yanaendelea kuanzisha uongozi wa matawi kabla ya kuruhusu uchaguzi wa Seneti kufanyika hapo baadaye.

Katika ngazi ya mikoa, mchakato wa kuchakata majina ya wagombea ulifanyika kupitia vikao vya Kamati za Uratibu za Seneti, vikihusisha viongozi mbalimbali wa Seneti na UVCCM. Vikao hivyo vilifuatiwa na Kamati za Utekelezaji za UVCCM mikoa, zilizojumuisha pia viongozi wa CCM ngazi ya mkoa.
Ngazi ya taifa, uamuzi wa mwisho ulifikiwa kupitia kikao maalum cha Kamati ya Utekelezaji ya Baraza Kuu la UVCCM Taifa kilichofanyika Februari 12, 2026. Kikao hicho kilitanguliwa na kikao cha Sekretarieti kilichofanyika Februari 10, 2026 katika Chuo cha UVCCM Tunguu, Zanzibar.

Hatimaye, vikao hivyo vilielekeza kuwa uchaguzi huo ufanyike nchi nzima Februari 14, 2026, hatua iliyotekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kukamilisha mchakato huo muhimu wa kidemokrasia ndani ya jumuiya hiyo ya vijana.




# DKT BUNUNGU ANG'ARA UCHAGUZI MDOGO PERAMIHO, VIJANA CCM WATAMBA NA ILANI YA MAENDELEO

Na Mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Jimbo la Peramiho ni miongoni kati ya majimbo 272 ya Uchaguzi nchini Tanzania, ni Jimbo lenye Jumla ya Kata 16 zinazounda maeneo yake yote ya Uchaguzi na Usimamizi wa kisiasa Jimbo hili Linapatikana katika Wilaya ya Songea Mkoani Ruvuma

Mnamo tarehe 21 Januari 2026 Tume huru ya Uchaguzi (INEC) Ilitoa Tangazo la Kufanyika kwa uchaguzi mdogo jimboni Peramiho Kuziba nafasi iliyoachwa wazi kutokana na Kifo cha aliyekuwa mbunge wa Jimbo Hilo marehemu Mh. Jenista Mhagama
Kwa mujibu wa tangazo la uchaguzi lililotolewa na Tume Huru ya uchaguzi (Inec) walitoa ratiba ya kufanyika kwa Kampeni hivyo Kampeni zilifunguliwa rasmi mnamo tarehe 5 Februari 2026 mpaka tarehe 25 Februari 2026 na siku rasmi ya kufanyika uchaguzi huo Ikapangwa kuwa ni tarehe 26 Februari 2026 ambapo Jumla ya vyama 15 Vilisimamisha wagombea wao katika Kushiriki kampeni za Uchaguzi huo wa Ubunge na Kwa Upande wa Chama cha Mapinduzi CCM Walimsimamisha Dkt. Bunungu Lazaro Komba kuipeperusha bendera ya CCM kwa nafasi ya Ubunge Jimboni Hapo





Siku ya Alhamisi 26 Februari, 2026 wananchi wengi wapiga kura waliojiandikisha walijitokeza katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kitimiza haki yao ya kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa katika nafasi za Uongozi ambapo kwa Mujibu wa Taarifa Zilizotolewa na Tume Huru ya Uchaguzi (INEC), vyama vilivyoshiriki Uchaguzi Mdogo vilikuwa vyama 15 .

Aldha, jumla ya wapiga kura walioandikisha ni 120780 ambapo waliojitokeza kupiga kura ni 79,313 sawa na 66% ya wapiga kura wote wa Jimbo la Peramiho.
Mgombea wa Ubunge kwa tiketi ya CCM Dkt. Bunungu Lazaro Komba aliibuka kidedea Kwa kura za ushindi 69,002 sawa na 87% ya wapiga kura wote waliojitokeza siku hiyo.
Kupitia Sera, Ahadi na Nia ya dhati katika Kuwaletea watanzania Maendeleo CCM Imedhamiria pia imeweka mkataba na wananchi kupitia uwepo wa ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025/30 Ambapo imeelezea Kwa kina namna na Hatua za kufuata katika kuyaleta maendeleo hayo ili kuhakikisha inakuza Uchumi na kipato Kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kiujumla ili kutimiza kiu ya wananchi na Taifa katika kuhakikisha maendeleo endelevu yanapatikana na Taifa linasonga mbele siku zote







MAKALA MAALUMU

# SIKU 100 ZA DKT. SAMIA ZIMELETA FURSA NA MATUMAINI KWA VIJANA WA KITANZANIA



Na Jessica Mshama,
Katibu wa Idara ya Uhamasishaji
na Chipukizi - UVCCM Taifa

## *Asili ya Dhana ya Siku 100 za Uongozi*

Dhana ya "siku 100" katika uongozi haikutokea ghafla, bali ni matokeo ya somo kubwa la kihistoria lililotokana na wakati mgumu ambao ulilazimisha kiongozi kuonyesha uwezo wake ndani ya muda mfupi. Chanzo cha siku 100 ni uongozi wa Franklin D. Roosevelt mwaka 1933, alipoapishwa kuwa Rais wa 32 wa Marekani katika kipindi ambacho dunia ilikuwa imegubikwa na mdororo mkubwa wa uchumi (Great Depression). Marekani wakati huo ilikuwa katika hali ya sintofahamu ikikubwa na changamoto za kiuchumi, matumaini ya wananchi yakizidi kufifia.

Ni katika mazingira hayo ndipo Roosevelt alipoamua kuuvunja ukimya wa hofu kwa vitendo. Badala ya kusubiri muda mrefu kuonyesha mwelekeo wa uongozi wake, aliingia kazini mara moja kwa kasi ya ajabu.

Ndani ya kipindi cha siku 100 tu, aliwasilisha na kufanikisha kupitishwa kwa sheria na sera zenye tija kupitia Bunge la Marekani, hatua zilizokuja kujulikana kama New Deal. Ndani ya siku 100 alikuwa ameshatoa majibu ya haraka kwa kilio cha wananchi akirejesha ajira, kuimarisha taasisi za kifedha na zaidi ya yote, kurudisha imani ya wananchi kwa serikali yao.

Katika hotuba yake ya kuapishwa, Roosevelt alitamka maneno ambayo yameendelea kunukuliwa na wachambuzi wa siasa na uongozi duniani hadi leo:

"The only thing we have to fear is fear itself."
Franklin D. Roosevelt, Inaugural Address, 1933

Tafsiri yake kwa Kiswahili ni kwamba kitu pekee kinachopaswa kuwatisha watu sio hali halisi waliyonayo, bali ni hofu inayowafanya washindwe kuchukua hatua ndipo dhana ya "siku 100" ikazaliwa kama falsafa ya uongozi. Ilianza kuonekana kuwa kipindi cha siku 100 kinaweza kupima mwelekeo wa Uongozi: je, ana dira? ana uthubutu wa kufanya maamuzi magumu
yenye kulete faida kwa Taifa.

Kadri miaka iliyoendelea viongozi na marais wa mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania walianza kuitumia dhana ya Siku 100 kama kioo kinachoonyesha taswira ya mwanzo ya uongozi, kasi ya utekelezaji, uwezo wa kupanga vipaumbele na dhamira ya kweli ya kuwatumikia watanzania.

## *Siku 100 za Samia Suluhu Hassan na Uongozi wenye Matokeo na Matumaini kwa Vijana*

Kwa upande wa taifa letu, siku 100 za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan zimejitokeza kama alama ya mageuzi Chanya kwa taifa, yenye mwelekeo na mguso wa moja kwa moja kwa maisha ya wananchi. Ni siku zilizobeba matumaini mapya, zikifungua milango ya fursa na kuamsha imani ya Watanzania hasa vijana, ambao kwa zaidi ya asilimia 60 ya idadi ya watu, ndio mhimili mkuu wa leo na kesho wa taifa letu.

Uongozi wake umejengwa juu ya msingi wa kusikiliza, kutenda na kujali, ukionesha wazi kuwa maendeleo ya taifa hayawezi kufikiwa bila kuwaweka vijana mstari wa mbele.

Katika kipindi hiki kifupi, dira yake imeonekana, sera zikihuishwa, ahadi zikitekelezwa na maisha ya wananchi yakianza kuguswa kwa namna inayoonekana na kupimika na kuleta faida.

*"Zaidi ya asilimia 60 ya watu wa nchi hii ni vijana; tutapanua fursa za kiuchumi, ajira na hifadhi ya jamii….."* Dkt. Samia Suluhu Hassan

## Uwekezaji Mkubwa kwa Vijana

Katika siku 100 za uongozi wa Samia Suluhu Hassan, dhana ya kuwaweka vijana mbele imepata tafsiri halisi ya vitendo. Uamuzi wa kuanzishwa kwa Wizara ya Vijana umefungua ukurasa mpya wa maendeleo, ukionesha wazi kuwa serikali imechagua kwa makusudi kuwekeza katika nguvu kazi ya taifa. Kupitia hatua hii, vijana wameanza kunufaika na fursa za mafunzo ya ujuzi wa kisasa na teknolojia, programu za ujasiriamali zinazowawezesha kuanzisha na kukuza biashara, pamoja na mifumo rafiki ya kujiajiri inayowapa uhuru wa kiuchumi. Ukweli kwamba asilimia 46 ya ahadi zote ndani ya siku 100 zililenga moja kwa moja vijana unaonesha dhamira ya dhati ya uongozi huu kwamba vijana sio watazamaji wa maendeleo, bali Vijana ndio wahusika wakuu wa safari ya Maendeleo ya taifa letu.

## Mapinduzi katika Sekta ya Afya

Katika kuimarisha ustawi wa jamii, serikali imechukua hatua za kihistoria kuboresha huduma za afya kwa namna inayogusa maisha ya wananchi wa kawaida. Uzinduzi wa Bima ya Afya kwa Wote (katika majaribio) umeanza kuwafikia makundi yasiyo na uwezo, huku zaidi ya wananchi milioni 1.4 wakianza kunufaika na mfumo huo. Bajeti ya shilingi bilioni 48.8 iliyotengwa imewezesha upatikanaji wa huduma, na zaidi ya wagonjwa milioni 1.4 wamepata matibabu ya bure kwa magonjwa makubwa. Aidha, uamuzi wa kupiga marufuku hospitali kuzuia miili ya marehemu kwa sababu ya madeni umeirejesha hadhi ya utu wa Mtanzania. Haya yote yanaonesha wazi kuwa uongozi huu unajali afya na pia heshima ya maisha ya mwananchi.

## Ajira kwa Vijana na Kuinua Sekta za Afya na Elimu

Katika kukabiliana na changamoto ya ajira na kuboresha huduma za kijamii, serikali imechukua hatua madhubuti katika sekta za afya na elimu. Zaidi ya wahudumu wa afya 4,525 tayari wameajiriwa kati ya waliopangwa 5,000, huku ajira za walimu wa sayansi na hisabati zikifikia 6,044 kati ya 7,000 waliokusudiwa. Hatua hizi zimeongeza ufanisi katika utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi, lakini pia zimefungua milango ya ajira kwa maelfu ya vijana wasomi. Huu ni ushahidi kuwa maendeleo ya sekta hizi yanaenda sambamba na uwezeshaji wa vijana awakipewa nafasi ya kulitumikia taifa lao huku wakijijengea maisha bora.

## Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Vijana

Ahadi ya serikali ya kutenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwawezesha vijana na hasa wajasiriamali wadogo wadogo imeanza kuzaa matunda ndani ya muda mfupi. Zaidi ya wajasiriamali milioni 1.1 wametambuliwa na maelfu tayari wameanza kusajiliwa rasmi na kunufaika na mikopo ya riba nafuu. Hatua hii imeanza kuibadilisha sekta isiyo rasmi kuwa nguvu rasmi ya uchumi, huku vijana wengi wakipata mitaji ya kuanzisha na kukuza biashara zao. Huu ni uongozi unaowajengea vijana uwezo wa kujitegemea, badala ya kusubiri ajira ukiwawezesha kuwa wabunifu wa fursa na wachangiaji wakuu wa uchumi wa taifa.



## Viwanda na Ajira ili Kujenga Uchumi wa Ndani

Kupitia mpango wa kongani za viwanda wilayani, serikali imeanza kuweka msingi imara wa uchumi wa viwanda unaotegemea rasilimali za ndani. Tathmini iliyofanyika katika mikoa mbalimbali kama Dodoma, Mbeya, Morogoro na Kigoma inalenga kubaini fursa za uzalishaji na kuongeza thamani ya mazao ya ndani. Mpango huu unafungua milango mipya ya ajira kwa vijana, huku ukiwawezesha kushiriki moja kwa moja katika uzalishaji na uchakataji wa bidhaa. Ni hatua inayojenga Tanzania inayojitegemea kiuchumi, huku vijana wakichukua nafasi yao kama injini ya maendeleo ya viwanda.

## Kuandaa Vijana kwa Uchumi wa Kidijitali

Kwa kutambua kasi ya dunia kuelekea uchumi wa maarifa na teknolojia, serikali ya Samia Suluhu Hassan imechukua hatua za kimkakati kupitia mpango wa Samia Scholarship Extended (SSE DS/AI+), unaolenga kuwajengea vijana uwezo wa ushindani wa kimataifa. Kupitia mpango huu, tayari vijana 20 wamepata ufadhili wa masomo ya juu katika taaluma za kisasa kama Data Science, Artificial Intelligence (AI) na teknolojia shirikishi wakiwa wamepangiwa kusoma katika taasisi zenye hadhi ya juu kama Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) na Indian Institute of Technology Zanzibar.

Ingawa idadi hii ni ya awali, inaashiria mwanzo wa safari pana ya uwekezaji katika rasilimali watu, hasa vijana wenye vipaji na uwezo mkubwa. Kwa kutenga shilingi bilioni 5 kwa ajili ya mpango huu, serikali inaweka msingi imara wa kujenga kizazi kipya cha wataalam wa teknolojia na ubunifu, watakaoliwezesha taifa kushindana katika uchumi wa kidijitali. Huu ni uwekezaji unaoonesha maono ya mbali kuwaandaa vijana wa Kitanzania sio kwa soko la ajira la leo tu, bali kwa dunia ya kesho inayotawaliwa na maarifa na teknolojia.



## Uongozi wenye Matumaini

Kwa ujumla, siku 100 za Rais Samia Suluhu Hassan zimejidhihirisha kuwa ni ushahidi wa uongozi unaojali, unaosikiliza na unaotekeleza kwa vitendo. Mafanikio haya yanaweka msingi wa taifa lenye uchumi shindani, jamii jumuishi na vijana wenye matumaini mapya. Kwa hakika, kipindi hiki kifupi kimeacha alama isiyofutika, kikithibitisha kuwa uongozi bora haupimwi kwa muda pekee, bali kwa ubora wa maamuzi na kasi ya kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya wananchi.Sisi Vijana wa kitanzania tuna matumaini na imani na Rais Dkt. Samia Kiongozi wa maendeleo.




# RAIS DKT. SAMIA MDAU NAMBA 1 WA MICHEZO NCHINI ALIYEILETA SAHANI YA AFCON NYUMBANI

Na Mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Kenya na Uganda imefanikiwa kushinda zabuni ya kuandaa mashindano ya Afcon kupitia "Pamoja Bid" ambapo nchi hizi zote tatu za Africa mashariki zilishirikiana katika Uombaji wa tenda ya zabuni hio na kushinda hivyo wamepata nafasi ya kufanya maandalizi pamoja na kufanikisha mashindano ya michezo hiyo ya Afcon 2027 katika nchi husika.



***Juhudi na hatua za Rais Dkt. Samia katika kuikuza sekta ya michezo nchini***

Ni wazi kuwa Rais Dkt. Samia amesaidia kwa kiasi kikubwa sana maendeleo ya michezo nchini kuanzia ngazi ya chini ya mitaa kwa michezo ya aina zote, kwenda ngazi za vilabu mpaka kitaifa

***Hatua alizochukua ni Pamoja na;***

1. Ameinua maendeleo ya timu za klabu nchini kupitia zawadi za kifedha katika kampeni ya Goli la Mama. Kupitia kampeni hii imehamasisha sana wachezaji pamoja na timu za klabu mbalimbali nchini ikiwemo timu ya Taifa 'Taifa Stars' katika kujituma kikamilifu na

kutafuta ushindi ambapo Rais Dkt. Samia amekuwa akiwaahidi na kutoa fedha taslimu kupitia ushindi wa timu.

2. Ongezeko la Bajeti ya michezo kila mwaka kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/26 bajeti ya wizara imeongezeka kufikia Bilioni 519.66 kutoka Bilioni 285.3 ya mwaka 2024/25 hivyo kupelekea ongezeko la ufanisi katika utendaji wa sekta ya michezo.

3. Rais Dkt. Samia ametambua na kuwapongeza wanamichezo walipofanya vizuri na kuwatia moyo waliposhiriki mashindano ya kimataifa ambapo amekuwa akiwapongeza hadharani wanamichezo wanaoiletea taifa heshima kupitia mikutano na hafla maalum, jambo ambalo linaongeza motisha kwa wanamichezo wengine.

4. Rais Dkt. Samia amelikuza soka la ndani na kuzisaidia klabu vinavyoiwakilisha Tanzania kimataifa kama Yanga na Simba kwa kuviwezesha katika namna mbalimbali za kuvifanya visonge mbele kimataifa.

5. Uanzishwaji wa Samia Cup, Ndondo Cup, Mhola Mia Cup n.k ni mashindano ya michezo yenye lengo la kukuza vipaji vya vijana na kuikuza sekta ya michezo nchini.






*Juhudi na hatua za Rais Dkt. Samia kulipeleka soka na michezo ya Tanzania Kimataifa*

1. Kufanikiwa kushinda zabuni ya Kuandaa Afcon 2027 ni moja wapo ya mafanikio makubwa yatakayosaidia Utalii wa Michezo hapa nchini pamoja na fursa mbalimbali ikiwemo ajira pamoja na kukua kwa uchumi wa Mtanzania mmoja mmoja pamoja na wa kitaifa.

2. Amekutana na viongozi wakubwa wa michezo, wamiliki wa vilabu vya michezo vinavyoongoza kimataifa pamoja na wachezaji wa sekta hiyo ya michezo kwa lengo la kujenga uhusiano wa michezo ya Tanzania Kimataifa ambapo tarehe 11 Aprili 2025 Rais Dkt. Samia alikutana na Sir Jim Ratcliffe mmiliki mshirikishi wa klabu kubwa duniani ya Manchester United, pia mnamo tarehe 19 Novemba alikutana na Rais wa CAF, Ndugu Patrice Motsepe.

3. Ukarabati wa ujenzi wa viwanja vikubwa vya michezo ili kukidhi viwango vya shirikisho la soka Afrika ambapo Uwanja wa Benjamin Mkapa umeendelea kufanyiwa marekebisho makubwa. Uwanja wa New Amaani Complex umejengwa upya kwa kiwango cha kimataifa pamoja na ujenzi wa Uwanja wa Samia Suluhu Hassan Uliopo Jijini Arusha utakaogharimu Kiasi cha shilingi Bilioni 286 Uwanja utakaokidhi viwango vya kimataifa.





4. Uboreshaji wa miundombinu pamoja na kuboresha mazingira ya utalii kuelekea AFCON 2027. Rais Dkt. Samia ameielekeza serikali kuhakikisha inawekeza kwenye barabara zote, viwanja vya ndege, Hoteli ,na huduma za utalii pamoja na Usafiri wa mashabiki hii itasaidia kuhakikisha wageni kutoka Afrika na Dunia wanapata huduma bora pamoja na kufurahia vivutio vya utalii kitu kitakachoongeza thamani na kukuza uchumi wa nchi.

5. Kutokana na Juhudi za" Michezo ya Tanzania Kimataifa Rais Dkt. Samia amepokea Tuzo Maalum ya CAF President's Outstanding Achievement's Awards 2025 Ilitofanyika Rabat Nchini Morocco.

6. Rais Dkt. Samia Mnamo Tarehe 14 Agosti 2025 alipokea Medali ya Heshima kutoka Shirika la International Military Sports Councill (CISM) kwa kuchangia maendeleo ya michezo na amani kupitia michezo. Tukio hili lilidhihirisha uhusiano wake na taasisi hii ya michezo duniani na kuthibitisha ushawishi wake wa kimataifa.















# Buriani

## WILLIAM VANGIMEMBE LUKUVI
## 1955-2026

Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) chini ya uongozi wa Mwenyekiti Ndugu Mohammed Ali Kawaida (MCC), tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Ndugu William Vangimembe Lukuvi (MB), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu) pamoja na Mbunge wa Jimbo la Isimani.

Kifo chake ni pigo kubwa sio tu kwa Serikali na Chama, bali pia kwa vijana waliokuwa wanufaika wa uzoefu, malezi na uongozi wake wa muda mrefu.

Marehemu Lukuvi alikuwa mtumishi wa umma mwenye uzoefu mpana tangu mwaka 1995, akihudumu katika nafasi mbalimbali za uongozi wa kisiasa na kiutendaji ambapo alijitambulisha kwa uadilifu, weledi na uzalendo wa hali ya juu katika kusimamia masuala ya maendeleo ya taifa letu.

Ndani ya UVCCM, Marehemu alikuwa nguzo muhimu katika historia ya nyakati za vijana akiwa ameshika nyadhifa mbalimbali zenye mchango mkubw katika kujenga na kuimarisha jumuiya ya UVCCM. Amehudumu katika nafasi ya Katibu wa UVCCM Wilaya (Masasi, Mtwara, Arusha na Dodoma), Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM pamoja na Kamati ya Utekelezaji ya UVCCM, Mkuu wa Idara ya Organaizesheni - UVCCM, Katibu wa UVCCM Mkoa wa Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM, na kadhalika.

UVCCM inamtambua Marehemu kama kiongozi mlezi, mwalimu wa vijana. Kuondoka kwake ni upotevu wa hazina ya maarifa, uzoefu wa hekima ambayo imekuwa mhimili wa maendeleo ya Vijana ndani ya CCM, Serikali na Taifa kwa ujumla.

Katika kipindi hiki kigumu, UVCCM inaungana na familia ya Marehemu, ndugu, jamaa, marafiki, wananchi wa Isimani pamoja na Watanzania wote katika kuomboleza msiba huu mzito.

Tunawaomba vijana wote nchini kuendeleza misingi, maadili na maono aliyoacha Marehemu, kuendelea kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa na kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi.

Ameen!



UMOJA WA VIJANA WA CCM

# KIJANA, KILIMO NI FURSA

## TUNAKODISHA VIFAA

- Power tiller
- Trekta
- Plau
- Vifaa vya Kuvunia Mpunga

Kodi Vifaa Bora vya Kilimo
**Kutoka kwa Mawakala wetu kwa Gharama ya Kizawa.**





Kuwa Sehemu ya **Vijana** wenye **Ndoto** na **Waliofanikiwa**

**Wasiliana Nasi:**
katibumkuuuvccm@ccm.or.tz
+255 716 277 814




# ASANTE KWA KUSOMA JARIDA LA VIJANA MAGAZINE

uvccm_tz // VIJANA TV

Kwa Maoni/ Ushauri

**+255 655 248 822**

**Kazi na Utu Tunasonga Mbele**